# KUISHI KWA IMANI

## UKUAJI WA KIKRISTO

**Na E. J. WAGGONER**

# KUISHI KWA IMANI

KATIKA Warumi 1:17, Mtume Paulo ***anatoa*** usemi huu, "Kwa maana ***haki*** ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ***ilivyoandikwa***, Mwenye haki ataishi kwa imani." Usemi huo ***ndio*** muhtasari wa kile alicho nacho Mtume huyo kusema juu ya Injili katika fungu la 16. Injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, lakini tu ni "kwa kila aaminiye," katika hiyo haki ya Mungu inayodhihirishwa. ***Haki ya Mungu ni ile Sheria kamilifu ya Mungu [Amri Kumi]*** (Isaya 51:6,7; Zaburi 119:172), ambayo ndiyo ***chapa [nakala halisi] ya mapenzi yake mwenyewe*** (Zaburi 40:7,8). Kila lisilo la haki ni dhambi (1 Yohana 5:17), au ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi] (1 Yohana 3:4, AJKK; Rum. 7:7). Injili ni tiba ya Mungu ya dhambi; kwa hiyo, kazi yake inapaswa kuwa ni ile ya kuwaleta watu katika hali ya mwafaka [yaani, kupatana] na Sheria hiyo [Amri Kumi], - yaani, kuwezesha utendaji wa Sheria hiyo ya haki [Amri Kumi] upate kudhihirika katika maisha yao. Lakini hiyo kabisa ni kazi ya imani, - haki ya Mungu inadhihirishwa "toka imani hata imani," - imani toka mwanzo, na imani mpaka mwisho, - kama ilivyoandikwa, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

Hilo ni kweli katika vizazi vyote tangu lilipotokea anguko la mwanadamu, tena litakuwa la kweli mpaka watakatifu wa Mungu watakapokuwa na jina lake katika vipaji vya nyuso zao, na kumwona yeye kama alivyo hasa. Ni kutoka kwa nabii Habakuki (2:4) ambako Mtume huyo alinukuu usemi huo. Kama manabii wale wasingekuwa wameifunua [kweli] hiyo, basi, Wakristo wale wa kwanza wasingeweza kuijua; maana walikuwa na Agano la Kale tu. Kusema kwamba katika zama zile za kale sana watu walikuwa na dhana isiyo kamilifu kuhusu imani katika Kristo, ni kusema kwamba hapakuwako na watu wenye haki katika nyakati zile. Lakini Paulo anakwenda mpaka mwanzo kabisa na kutaja mfano mmoja wa imani iokoayo. Anasema hivi, "Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki." Ebr. 11:4. Anasema juu ya Nuhu kwamba ilikuwa ni kwa imani alipounda safina ile na kuiokoa nyumba yake; "na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa ***haki ipatikanayo kwa imani***." Ebr. 11:7. Sisi tunasema kwamba imani yao ilikuwa ndani ya Kristo, kwa sababu ilikuwa ni imani iliyowaletea wokovu, na zaidi ya jina la Yesu "hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12.

Kuna wengi mno wanaojaribu kuishi maisha ya Kikristo kwa nguvu ya imani waliyokuwa nayo walipotambua haja yao ya kupewa msamaha kwa dhambi walizotenda katika maisha yao ya zamani. Wanajua kwamba ni Mungu peke yake awezaye kusamehe dhambi na kwamba yeye anafanya hivyo kwa njia ya Kristo; lakini wao wanawaza kwamba, kama walikuwa wamekwisha kuanza zamani [kwa imani], basi, wanapaswa kukimbia mbio hizo kwa nguvu zao wenyewe. Tunajua kwamba wengi wanayo dhana

hiyo, kwanza, kwa kuwa tumekwisha kuwasikia baadhi yao wakisema hivyo, na, pili, kwa sababu ya watu wengi kama hao wanaojiita Wakristo ambao huonyesha utendaji wa nguvu isiyozidi ile yao wenyewe. Kama wanalo lo lote la kusema katika mikutano ya ushuhuda, kando ya kanuni hii inayojirudia yenyewe tena na tena, isemayo, "Mimi nataka kuwa Mkristo, ili nipate kuokolewa," basi, wao husimulia tu uzoefu wao wa maisha yao yaliyopita, na furaha waliyokuwa nayo walipoamini mara ya kwanza. Kuhusu kuishi kwa ajili ya Mungu, na kutembea naye kwa imani, wao hawajui kitu, na ye yote anayewaambia juu ya jambo hilo anasema lugha ngeni kwao. Lakini Mtume huyo analiendeleza jambo hilo la imani mpaka kufika katika ufalme ule wa utukufu, kwa kielelezo chenye nguvu kabisa kifuatacho:-

"Kwa imani Henoko alihamishwa, asije akaona mauti, wala hakuonekana, kwa sababu Mungu alimhamisha; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu. ***Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao***." Ebr. 11:5,6.

Zingatia hoja hiyo inayothibitisha kwamba Henoko alihamishwa kwa sababu ***alitembea na Mungu na kushuhudiwa kwamba amempendeza Mungu***. Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza. Hayo yatosha kuthibitisha pointi hiyo. Pasipo imani hakuna tendo lo lote liwezalo kufanywa ambalo linaweza kupata kibali cha Mungu. Pasipo imani matendo mema kabisa awezayo kufanya mtu yatapungua kabisa kuifikia haki ya Mungu iliyo kamilifu, ambayo peke yake ndiyo kipimo chetu. Po pote pale ambapo imani ya kweli inaweza kupatikan a, ni jambo jema; lakini imani bora kabisa ndani ya Mungu inayoweza kuziondolea mbali dhambi zilizopita, haitamfaidia kitu mtu ye yote mpaka iendelezwe kwa kiwango kinachoongezeka daima mpaka mwisho wa kipindi chake cha majaribio [yaani, cha kupimwa tabia yake].

## SABABU YA KUSHINDWA

Tumekwisha kuwasikia watu wengi wanaosimulia jinsi ilivyokuwa vigumu kwao kufanya mema; maisha yao ya Kikristo yalikuwa hayaridhishi kabisa kwao, yakiwa na dalili ya kushindwa tu, tena walijaribiwa ***kuacha kujitahidi kwa kukata tamaa kwao***; kushindwa kule kunakoendelea daima kunatosha kumkatisha tamaa mtu awaye yote. Askari shujaa kuliko wote ulimwenguni angekuwa mwoga kama angekuwa ameshindwa katika kila pambano. Wakati mwingine watu hao wanaomboleza na kusema kwamba karibu wameipoteza imani yao kabisa. Lakini kama wangekuwa wameipoteza imani yao yote ya kujitegemea wenyewe tu, na kama wangeweka tumaini lao lote ndani ya yule Mmoja aliye na uweza wa kuokoa [yaani, Kristo], basi, wangekuwa na habari tofauti ya kusimulia. Ndipo wao wange"furahi katika Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. Asema hivi huyo Mtume, "Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini." Wafilipi 4:4. Mtu yule asiyefurahi katika Mungu, hata kama anajaribiwa na kuteswa, hapigi vita vile vizuri vya imani. Anapiga vita vibaya vya ***kujiamini mwenyewe*** na [matokeo yake ni] kushindwa.

Ahadi zote za furaha ile ya mwisho zinatolewa kwa mshindi [tu]. "Yeye ***ashindaye***," asema Yesu, "nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi ***nilivyoshinda*** nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi." Ufunuo 3:21. "Yeye ***ashindaye*** atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa

mwanangu." Ufunuo 21:7. Mshindi ni yule anayejipatia ushindi. Urithi wenyewe sio ushindi; ni zawadi tu ya ushindi. ***Ushindi ni SASA***; ushindi unaotakiwa kupatikana [sasa] ni ***ushindi juu ya tamaa za mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima -*** yaani, ***ushindi juu ya nafsi na mambo ya ubinafsi tunayojiendekeza [tunayojiachilia tu] kufanya***. Mtu apiganaye na kumwona adui yake akishindwa, anaweza kufurahi; hakuna mtu anayeweza kumzuia asifurahi, maana furaha huja yenyewe kama matokeo ya kumwona adui akishindwa. Watu wengine hutazamia kwa hofu kuu wazo hilo la ***kupigana vita daima*** dhidi ya nafsi zao na tamaa za dunia hii. Hii ni kwa sababu wao bado hawajui kitu juu ya furaha inayopatikana katika ushindi; wamepata uzoefu wa kushindwa tu. Lakini hilo si jambo la kuhuzunisha mno kuendelea kupigana daima ikiwa ushindi wa daima unaweza kupatikana. Askari mkongwe mstaafu aliyepigana vita mia moja, ambaye alikuwa mshindi katika kila vita, hutamani kuwa katika eneo la vita. Askari wale wa Iskanda (Alexander), ambao chini ya amri yake hawakujua kamwe kushindwa, walikuwa wepesi sikuzote kuongozwa katika mapigano. Kila ushindi walioupata uliwaongezea nguvu, ambayo hiyo ilitokana na ujasiri wao tu, na kwa ulinganifu waliweza kuipunguza [nguvu] ya adui yao aliyeshindwa. Basi, sisi twawezaje kujipatia ushindi wa kudumu katika vita yetu hii ya kiroho? Hebu na tumsikilize mwanafunzi yule mpendwa:-

"Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu ***huushinda ulimwengu***; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo ***imani*** yetu." 1 Yohana 5:4.

Someni tena maneno haya ya Mtume Paulo:-

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala ***si mimi tena*** [umimi umekufa], bali ***Kristo yu hai ndani yangu***; na uhai nilio nao sasa katika mwili ninao katika ***imani*** ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." Wagalatia 2:20.

Hapa ndipo ilipo ***siri ya kupata nguvu***. Ni ***Kristo***, Mwana wa Mungu, yaani, yule Mmoja aliyepewa mamlaka yote mbinguni na duniani, ambaye ***ndiye atendaye kazi [ndani yetu]***. Kama yeye anakaa ndani ya moyo wetu kutenda kazi yake, je! ni kujisifu kusema kwamba ushindi wa daima unaweza kupatikana? Naam, huko ni kujisifu; lakini ni kujisifu katika Bwana, na jambo hilo linaruhusiwa. Asema Mtunga Zaburi, "Katika BWANA nafsi yangu itajisifu;" na Paulo naye asema hivi, "Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu." Wagalatia 6:14.

Askari wale wa Iskanda (Alexander) walidhaniwa kwamba hawashindikani. Kwa nini? Je, ilikuwa ni kwa sababu walikuwa na nguvu nyingi za kuzaliwa nazo na wajasiri kuliko maadui zao wote? - La, ila ni kwa sababu waliongozwa na Iskanda. Nguvu zao zilitegemea uongozi wake. Chini ya kiongozi mwingine wangekuwa wameshindwa mara nyingi. Jeshi la Muungano, likawa linakimbia na kushikwa na hofu kuu na kuchanganyikiwa mbele ya adui yao kule Winchester, kule kuwapo kwake Sheridani kuliweza kugeuza kushindwa kwao kuwa ushindi. Bila kuwapo yeye, watu wale walikuwa ni kundi la watu waliokuwa wanatetemeka kwa hofu kuu; yeye alipojitupa mbele yao, wakawa jeshi lisiloshindikana. Ungekuwa umeyasikia maneno ya askari wale waliopigana chini ya viongozi wale wawili waliofanana, baada ya pambano lile kuisha, ungekuwa umesikia sifa zao kwa jenerali wao, zikichanganyika na shangwe yao yote. Walikuwa na nguvu kwa sababu yeye [kiongozi wao] alikuwa na nguvu; walichochewa kwa roho ile ile aliyokuwa nayo.

KIONGOZI WETU MWENYE NGUVU

Naam, Kapteni [Kamanda] wetu ni Bwana wa majeshi. Amewahi kupambana na adui yetu mkuu kuliko wote [Shetani] na ***kumshinda*** akiwa peke yake. Wale wanaomfuata yeye husonga mbele sikuzote ***wakishinda na kushinda***. Laiti kama wale wanaodai kuwa ni wafuasi wake wangeweka tumaini lao ndani yake, na, kisha, kwa ushindi tena na tena ambao wangeupata, wangeweza kuzitangaza sifa zake yeye aliyewaita kutoka gizani na kuingia katika nuru yake ya ajabu!

Yohana anasema kwamba yule aliyezaliwa na Mungu anaushinda ulimwengu kwa imani yake. Imani inaushikilia mkono wa Mungu, na uweza wake wenye nguvu unatenda kazi. Ni kwa jinsi gani uweza huo wa Mungu unaweza kutenda kazi yake ndani ya mwanadamu, kutimiza kile ambacho yeye [mwanadamu] asingeweza kujifanyia mwenyewe, hakuna awezaye kueleza. Kwa mantiki hiyo, ingekuwa rahisi vivyo hivyo kueleza jinsi Mungu anavyoweza kumpa uhai yule aliyekufa. Asema hivi Yesu, "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho." Yohana 3:8. Jinsi Roho atendavyo kazi yake ndani ya mwanadamu ili kuzidhibiti tamaa zake mbaya za mwili, na kumfanya awe mshindi juu ya kiburi, wivu, na uchoyo [ubinafsi] wake, ajuaye ni Roho peke yake. Yatosha kwetu kujua tu kwamba kazi hiyo imefanyika, na tena itafanyika ndani ya kila mmoja anayetaka, zaidi ya mambo mengine yote, kwamba kazi hiyo ifanyike ndani yake, kisha anamtumainia Mungu kuitenda kazi hiyo [ndani yake].

Sisi hatuwezi kueleza kwa jinsi gani Petro aliwezeshwa kutembea juu ya maji wakati mawimbi yalipokuwa yanaumuka kumzunguka pande zote; lakini tunajua kwamba kwa amri yake Bwana aliweza kufanya hivyo. Kadiri alivyozidi kukaza jicho lake kwa Bwana wake, ndivyo Uweza wa Mungu ulivyomwezesha kutembea kwa wepesi [juu ya maji yale] kana kwamba kulikuwa na mwamba mgumu chini ya miguu yake; lakini mara tu alipoyaangalia yale mawimbi, huenda akiwa na hisia ya majivuno moyoni mwake kwa kile alichokuwa akifanya, kana kwamba ni yeye mwenyewe aliyekuwa anafanya hivyo, basi, pasipo budi akajawa na hofu sana, na kuanza kuzama. ***Imani*** ilimwezesha kutembea juu ya mawimbi yale; ***hofu*** ikamfanya azame chini yake [yale mawimbi].

Asema hivi yule Mtume, "Kwa imani kuta za Yeriko zikaanguka, zilipokwisha kuzungukwa siku saba." Ebr. 11:30. Kwa nini mambo hayo yaliandikwa? - Kwa kutufundisha sisi "ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini." Rum. 15:4. Je! kuna matarajio yo yote kwamba sisi tutapata kuitwa kupigana na majeshi yenye silaha, na kuiteka miji yenye ngome? La; "kwa maana ***kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama [wanadamu]; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho***" (Waefeso 6:12); lakini ushindi ule uliokwisha kupatikana kwa imani katika Mungu juu ya maadui wanaoonekana katika mwili umewekwa katika kumbukumbu ili kutuonyesha sisi kile ambacho imani inaweza kufanya katika pambano letu dhidi ya wakuu wa giza wa ulimwengu huu. Neema ya Mungu, inayotolewa kwetu kama jibu la imani yetu, ina uwezo katika vita hizo [zisizoonekana] kama katika zile [zilizokuwa zikionekana]; kwa maana Mtume huyo anasema hivi:-

"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;

***tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo*.**" 2 Wakorintho 10:3-5.

Hawakuwa maadui wa kimwili tu ambao imani iliwawezesha wastahiki wale wa kale kuwashinda. Twasoma habari zao kwamba sio tu "walishinda milki za wafalme," bali "walitenda haki, walipata ahadi," tena, maajabu na mambo ya kutia moyo kuliko yote ni kwamba "***walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu***" (Ebr. 11:33,34). [Isa. 40:28-31.] Kwa imani udhaifu wao ule ule ukageuka na kuwa nguvu kwao, kwa kuwa uweza wake Kristo hutimilika katika udhaifu [1 Kor. 12:9,10]. "Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye ***kuwahesabia haki***, [Rum. 8:33]" "maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema" [Efe. 2:10]. "Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?" "Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda." Rum. 8:35,37.

## TOKA IMANI HATA IMANI

Lakini upo usemi mwingine katika fungu lile linalosimama mwanzoni mwa kijizuu hiki, usemao, "Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka ***imani hata imani***." Usemi huo ni somo lililojadiliwa sana kitaalam na wanatheolojia, na wachache mno miongoni mwao wanakubaliana kuhusu maana yake. Ukweli kwamba wasomi hao hawakubaliani kuhusu maana yake usitufanye sisi kuingiwa na hofu juu yake kwa wazo kwamba hauwezi kufahamika, maana tunasoma kwamba mambo yaliyofichwa kwa wenye hekima na akili yamefunuliwa kwa watoto wachanga [yaani, watu walio wachanga wa imani]. Ikiwa sisi tunakuwa wepesi kiasi cha kutosha kuikubali maana iliyotolewa wazi na Maandiko, yaani, kama inavyofafanuliwa na Maandiko, basi, sisi hatuna haja ya kubaki gizani.

Moja wapo ya sababu kuu kabisa zinazowafanya watu kushindwa kukielewa kitabu hiki cha Warumi, ni kushindwa kwao kuzishikilia kanuni za kwanza na maelezo yanayotolewa na Biblia. Watu wanajaribu kufafanua maneno fulani kulingana na mafunzo yao ya theolojia waliyoyapata [chuoni], na kuona kuwa ni kazi ngumu kuyafanya yaweze kutoa ufafanuzi unaofaa. Tena, ikiwa kwa wakati mmoja wameukubali ufafanuzi wa Biblia wa neno hilo, basi, huwa hawaushikilii ufafanuzi huo, bali hulipa [neno hilo] maana nyingine yo yote mahali hapo wakati watakapokutana nalo wakati mwingine. Jambo hilo haliwezi kuleta kitu cho chote ila machafuko tu.

Kiini cha ugumu wa kulielewa fungu hilo kinatokana na kushindwa kuushikilia sana ufafanuzi wa Biblia wa neno hili "***haki ya Mungu***." Tayari tumekwisha kuona ya kuwa ni usemi unaoonyesha ***tabia ya Mungu***, na ya kwamba ***tabia yake [Mungu] imefafanuliwa katika Amri Kumi***. Hizo zinatoa ***jumla ya wajibu wote umpasao mwanadamu***, yaani, ***kufanana na Mungu***. "Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu ***nawe uzishike amri zake [kumi]***, maana ***kwa jumla ndiyo impasayo mtu***. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya" (Mhubiri 12:13,14). "Lakini mkiitimiza Sheria ya Kifalme kama ilivyoandikwa, Mpende jirani yako kama nafsi yako, mwatenda vema…. Semeni ninyi, na kutenda kama ***watu watakaohukumiwa kwa Sheria ya Uhuru [Amri Kumi]***" (Yakobo 2:8,12). Sheria hiyo [Amri Kumi – soma fungu la 10,11], baada ya kuvunjwa, kwa kweli, haiwezi kuonyeshwa kikamilifu katika maisha ya mwanadamu

ye yote, na kwa ajili hiyo, Injili ilibuniwa [na Mungu] ili mwanadamu akiwa ndani ya Kristo apate kuwa na haki kamilifu ya sheria hiyo. Injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa kuwa inaifanya haki ya Mungu ipate kudhihirika. Sio tu kwamba inahubiriwa Sheria hiyo [Amri Kumi] - yaani, haki ya Mungu -, na uzuri wake kuinulia juu kwa njia ya Injili, bali kwa Injili hiyo matunda ya haki hufanywa yapate kuonekana katika maisha ya yule aaminiye.

Wengine wangetaka "haki ya Mungu" (righteousness of God) katika fungu hilo kuwa sawa na "kuhesabiwa haki (justification)." Hilo ni sawa, iwapo hawataliwekea mipaka fungu hilo kuihusu dakika ile tu ya kuhesabiwa haki mbali na dhambi zile za zamani. Ni kule kuitumia Sheria [Amri Kumi] iliyo ndani ya Kristo katika maisha ya mwenye dhambi [mvunjaji wa Amri Kumi] huyo kunakomhesabia haki. Kwa njia ya ukombozi ulio ndani ya Kristo Yesu, Mungu kwa neema yake anayahesabu maisha yaliyopita ya mwenye dhambi aaminiye kuwa kana kwamba yalikuwa yanapatana na Sheria yake [Amri Kumi] kwa kila hali. "Ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho ***kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake***, kwa sababu ya ***kuziachilia*** katika ustahimili wa Mungu ***dhambi zote zilizotangulia kufanywa***" (Rum. 3:25). Huko ndiko ***kuhesabiwa haki***. ***Ni ufunuo au udhihirisho*** wa haki ya Mungu kwa njia ya Injili. "Lakini sasa, haki ya Mungu inadhihirika pasipo Sheria [Amri Kumi]; inashuhudiwa na torati [Sheria/Amri Kumi] na manabii; ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti" (Rum. 3:21,22). Lakini fungu hilo linasema, "inadhihirishwa … toka imani hata imani;" na hilo haliwezi kumaanisha kitu kingine cho chote isipokuwa ile kazi ya haki inayoendelea hatua kwa hatua [ndani yetu]. Fungu hilo hufundisha kwamba haki ya Mungu inadhihirishwa kutoka hatua moja ya imani na kwenda hatua ya juu zaidi ya imani, na matokeo yake ni kwamba haki hiyo haina budi kuongezeka daima. Jambo hilo linaonyeshwa kwa njia ya dondoo analotoa Mtume huyo ili kuuthibitisha usemi wake. Ni lazima haki ya Mungu idhihirishwe toka imani hata imani, anaitoa hoja yake hiyo kwa sababu imeandikwa, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

## UKUAJI WA KIKRISTO

Nguvu yake inapatikana katika ukweli kwamba maisha ya Kikristo, ambayo hutokana na imani, ni maisha ya kusonga mbele hatua kwa hatua. ***Maisha ya Kikristo ni ukuaji unaoendelea daima***. Petro anasema: "Jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu, mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu. Lakini ***kueni katika Neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo***" (2 Petro 3:17,18). Njia pekee ya kujilinda nafsi zetu tusianguke na kukiacha kile tulicho nacho ni ***kukua***. Kuhusu mtu yule mwenye haki, Daudi anasema kwamba "atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji." Zaburi 1:3. Hii humaanisha ukuaji unaoendelea daima.

Tunasoma habari ya njia ya wenye haki kuwa "ni kama nuru ing'aayo, ***ikizidi kung'aa*** hata mchana mkamilifu [yaani, mpaka atakapokuja Yesu]." Mithali 4:18. Lakini "mwenye haki ataishi kwa imani;" basi, kwa mantiki hiyo, ni lazima imani yake izidi kuongezeka.

Tena: Paulo anawaambia Wakorintho maneno haya, "Na yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na ***kuzizidisha***, naye ***atayaongeza mazao ya haki yenu***." 2 Kor. 9:10.

Kwa Wathesalonike aliandika hivi: "Bwana na ***awaongeze na kuwazidisha*** katika upendo, ninyi kwa ninyi, na kwa watu wote." 1 Wathesalonike 3:12. Tena alisema, "Lakini twawasihi, ndugu zangu, ***mzidi sana***." 1 Wathesalonike 4:10. Lakini imani hutenda kazi yake kwa upendo (Wagalatia 5:6); yaani, upendo ni mmea unaokua kutokana na imani ya kweli; kwa hiyo, upendo unaozidi kuongezeka ni lazima uwe ni matokeo ya imani inayozidi kuongezeka.

Kwa Waebrania Mtume huyo aliandika hivi: "Kwa sababu hiyo, ***tukiacha kuyanena*** mafundisho ya kwanza ya Kristo, ***tukaze mwendo*** ili ***tuufikilie utimilifu***." Ebr. 6:1. Na katika waraka wake kwa Wafilipi, Paulo alisema hivi: "Si kwamba nimekwisha kufika au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali ***nakaza mwendo*** ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu, ***sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika***; ila natenda neno moja tu; ***nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo***, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu." Wafilipi 3:12-14. Hapa kumefafanuliwa kusonga mbele ili kukifikia kitu fulani unachotaka kukipata. Mwito wa Mungu katika Kristo Yesu ni mwito wa ***kuishi maisha matakatifu*** au ***maisha ya haki***, kwa maana twasoma maneno haya, "Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, ***Mtakuwa watakatifu*** kwa kuwa Mimi ni Mtakatifu." 1 Petro 1:15,16.

Haki hiyo tunayoitiwa, na mafanikio ya juu zaidi tunayotakiwa kujitahidi daima kuyapata, hupatikana kwa imani tu, kama Paulo alivyoeleza shauku yake ya kuonekana ndani ya Kristo, akiwa hana haki yake mwenyewe, "bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani." Wafilipi 3:9. Basi, kwa kuwa haki hiyo huja tu kwa imani, tena haina budi kuzidi kuongezeka, inafuata ya kwamba imani pia haina budi kuzidi kuongezeka. Hivyo halikuwa ombi la bure ambalo wanafunzi wake walitamka waliposema, "Bwana, Tuongezee imani." Luka 17:5.

Kwamba imani hiyo ina mwelekeo wa kukua imeelezwa waziwazi na Maandiko. Paulo alikuwa na tumaini kwamba imani ile ya ndugu zake Wakorintho itakapozidi kuongezeka, basi, angeweza kusaidiwa nao katika kuihubiri Injili katika nchi zile zilizokuwa mbele kupita nchi zao. "Wala hatujisifu zaidi ya kadiri yetu, yaani, katika taabu za watu wengine; bali tukiwa na tumaini ya kwamba, ***imani yenu ikuapo***, tutatukuzwa kwenu kwa kadiri ya kipimo chetu, na kupata ziada; hata kuihubiri Injili katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu; tusijisifu katika kipimo cha mtu mwingine kwa mambo yaliyokwisha kutengenezwa." 2 Kor. 10:15,16. Kwa Wathesalonike aliwaandikia kwamba aliomba sana usiku na mchana ili apate kuwaona, na kukamilisha kile kilichopungua katika imani yao. 1 The. 3:10. Na baadaye tena aliandika, akisema, "Ndugu, imetupasa kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, kama ilivyo wajibu, kwa kuwa ***imani yenu inazidi sana, na upendo*** wa kila mtu kwenu kwa mwenzake ***umekuwa mwingi***." 2 The. 1:3.

Fungu hilo la mwisho lina hoja yote tuliyokwisha kuitoa. Imani yao ilikua, na matokeo yake upendo wao ukawa mwingi. Fadhili au upendo ndio utimilifu wa Sheria [Amri Kumi]. Warumi 13:10; 1 Yohana 5:3. Ni udhihirisho wa haki ya Mungu, tena ni matokeo ya imani ya kweli, kwa maana imani hutenda kazi yake kwa upendo, na, haki peke yake itakayokubaliwa atakapokuja Bwana ni ile iliyo kwa imani katika Kristo, "haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani." Hayo yakiwa ndiyo mafundisho ya Maandiko,

hakuna sababu kwa nini tusingeweza kuelewa Warumi 1:17 kama isomekavyo, Haki ya Mungu inadhihirishwa au inafunuliwa,… toka imani hata imani.

Mfano mmoja au miwili hivi inayojulikana sana ambayo imeandikwa katika Maandiko itaweza kulielezea jambo hilo. Mtume huyo anaandika kwamba "Kwa imani Rahabu, yule kahaba, hakuangamia pamoja na hao walioasi, kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi kwa amani." Ebr. 11:31. Jambo hilo limekuwa sababu ya kujikwaza kwa wengine ambao hawajalitafakari kwa uangalifu. Ni jambo linalojulikana vizuri sana kwamba Rahabu alisema uongo kwa watu wale waliotumwa kwake na mfalme wa Yeriko kuwakamata wapelelezi wale (angalia Yoshua 2:2-6), basi, wao wanawaza kwamba katika kumwokoa huyo, Mungu alimshawishi kusema uongo, na ya kwamba wakati mwingine ni sawa kwa mtu kusema uongo. Mambo yote mawili si ya kweli. Rahabu aliokolewa, si kwa sababu ya uongo wake, bali kwa sababu ya imani yake. Yeye, kama watu wale wa kawaida wa Yeriko, alikuwa amekwisha sikia jinsi Bwana alivyoyakausha maji ya Bahari ya Shamu, na jinsi alivyowaongoza Waisraeli; lakini ni yeye peke yake, miongoni mwa wakazi wote wa Yeriko, aliyesadiki kwamba mkono wa Bwana ulikuwa katika jambo lile, na ya kwamba alikuwa amewapa Waisraeli nchi ile ya Kanaani. Alikuwa na imani ya kawaida tu, lakini alikuwa hajui kabisa juu ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Katika mfumo wa sheria za makafiri [wapagani], kusema uongo kulihesabiwa kama ni maadili mema, naye hakujua jema zaidi ya lile. Lakini imani yake ilifanya uwezekano uwepo kwa kuokolewa kwake, na kumleta mahali ambapo angeweza kujifunza haki. Kama matokeo ya kawaida imani yake kwa Mungu ingezidi kuongezeka kwa kadiri ambavyo angeendelea kujifunza zaidi juu yake. Katika suala lake tunacho kielelezo wazi cha udhihirisho wa haki ya Mungu toka imani hata imani.

Jambo lilo hilo ni kweli kumhusu Kornelio. Alikuwa anamcha Mungu pamoja na nyumba yake yote, na kutoa sadaka nyingi, na "kumwomba Mungu daima." Kama matokeo yake, malaika akatumwa kwake, akimwagiza kupeleka watu kumwita Petro, ambaye angemwambia yampasayo kutenda.

Jumla ya jambo zima ni kwamba ni imani inayomleta Mungu karibu nasi. Ikiwa sisi tutaamini kwanza ya kwamba yuko, basi, atajifunua kwetu yeye mwenyewe kwa ukamilifu zaidi. Tukifurahi katika nuru hiyo na kwenda katika hiyo, basi, imani yetu itazidi kuongezeka, na jambo hilo litazidi kutuletea sisi nuru nyingi zaidi. Kama ilivyokuwa kwa Rahabu, ndivyo ilivyo kwa wote. Mungu hatupi sisi mbaraka wake kwa kuwa sisi ni wenye haki, bali ili sisi tupate kuwa wenye haki. Imani yetu inapotuleta kwa Kristo, ni kwamba sisi tuweze kumjua yeye. Juu ya imani yetu, tunaongezea wema na maarifa. Lakini kwa vile imani huja kwa kusikia na kusikia huja kwa Neno la Mungu, basi, inafuata ya kwamba kadiri tunavyojua zaidi - yaani, kuendelea kulikubali -- Neno la Mungu, ndivyo imani yetu itakavyozidi kuwa kubwa zaidi. Basi, wakizidi kuongezeka katika imani yao, wenye haki husonga mbele toka nguvu hata nguvu, mpaka siku ile kamilifu itakapopambazuka na kuwaleta mbele zake Mungu.

E. J. Waggoner, ***Living By Faith (Christian Growth***.
Kiswahili – ***Kuishi Kwa Imani (Ukuaji Wa Kikristo)*** – translated by M. Mwamalumbili.